UN environment programme

# Ripoti ya UNEP ya Kukabiliana Na Pengo la Juhudi za Kukabiliana na Uzalishaji wa Gesi Chafu ya Mwaka wa 2024
## Ujumbe Muhimu

**Kadiri athari mbaya za tabianchi zinavyozidi kuongezeka, na kuumiza watu maskini duniani zaidi, *Ripoti ya UNEP ya Kukabiliana Na Pengo la Uzalishaji wa Gesi Chafu ya Mwaka wa 2024:* Liwe liwalo inaonyesha kuwa mataifa ni sharti yaimarishe juhudi za kukabiliana na hali, kuanzia na kujitolea kuchukua hatua kuhusu ufadhili katika COP 29.**

- Ongezeko la wastani la joto duniani linakaribia nyuzijoto 1.5 zaidi kuliko viwango vya kabla ya viwanda, na ubashiri wa hivi punde (kutoka kwa Ripoti ya Pengo la Uzalishaji wa Hewa Chafu ya mwaka wa 2024) ulionyesha ulimwengu unaelekea kushuhudia ongezeko hatari la nyuzijoto kati ya 2.6 na 3.1 karne hii isipokuwa tukishuhudia kupunguzwa kwa kiwango cha juu cha uzalishaji wa gesi ya ukaa haraka.
- Kwa hivyo kuna hitaji la dharura la kuimarisha kwa kiwango kikubwa kukabiliana na hali katika muongo huu ili kukabiliana na athari zinazoongezeka. Lakini hali hii inatatizwa na pengo kubwa lililopo kati ya mahitaji ya kifedha ya kukabiliana na hali na mtiririko wa sasa wa fedha za kimataifa za umma za kukabiliana na hali hii.
- Zinaposhuhudia hasara na uharibifu unaoongezeka, nchi zinazoendelea tayari zinapambana na kuongezeka kwa mzigo wa madeni. Ushughulikiaji madhubuti na wa kutosha wa hali, unaojumuisha haki na usawa, unahitajika kwa dharura zaidi kuliko hapo awali.
- Mataifa yanaweza kuimarisha ukabilianaji wa hali kwa kupitisha Lengo Jipya la Takwimu za Pamoja (NCQG) kapambe kwa ili kufadhili wa tabianchi katika COP 29 mjini Baku, Azerbaijan, na kujumuisha vipengele madhubuti vya kukabiliana na hali hii katika awamu inayofuata ya ahadi zao za kushughulikia tabianchi, au michango iliyoamuliwa na taifa, inayotarajiwa mapema mwaka ujao kabla ya COP 30 mjini Belém, Brazil.
- Kwa kuzingatia ukubwa wa changamoto, kuziba pengo la fedha za kukabiliana na hali pia kutahitaji mbinu bunifu na mambo wezeshi ya kukusanya rasilimali za ziada za kifedha.
- Mbali na fedha, kuna umuhimu wa kuimarisha ujengeaji uwezo na uhamishaji wa teknolojia ili kuboresha ufanisi wa hatua za kukabiliana na hali - hali inayorandana na kuzingatia mbinu za utekelezaji katika COP 29.
- Kwa ujumla, juhudi zaidi zitahitajika ili kufikia lengo la kimataifa la kukabiliana na hali kupitia shabaha kumi na moja za Mfumo wa Kustahimili Tabianchi Duniani wa UAE.

**Mitiririko ya fedha za kimataifa za umma za kukabiliana na hali unaongezeka, lakini bado kuna pengo kubwa kati ya kile kinachohitajika na kile kinachofanyika.**

- Mitiririko ya fedha za kimataifa za umma za kukabiliana na hali kwa nchi zinazoendelea iliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 22 katika mwaka 2021 hadi dola za Marekani bilioni 28 katika mwaka wa 2022: ongezeko kubwa kabisa la mwaka baada ya mwaka tangu wakati wa Mkataba wa Paris.
- Hali hii inaakisi hatua zilizopigwa kufikia Mkataba wa Tabianchi wa Glasgow, ambao ulihimiza mataifa yaliyoendelea angalau yaongeze maradufu fedha za kukabiliana na hali

kwa nchi zinazoendelea kutoka takriban Dola za Marekani bilioni 19 (viwango vya mwaka wa 2019) kufikia mwaka wa 2025.
- Hata hivyo, hata kufikia lengo la Mkataba wa Tabianchi wa Glasgow kunaweza tu kupunguza pengo la kifedha la kukabiliana na hali, ambalo linakadiriwa kuwa dola za Marekani kati ya bilioni 187 na bilioni 359 kwa mwaka, kwa takriban asilimia 5.

## Upangaji na utekelezaji wa ukabilianaji wa hali kwa ujumla unaongezeka, lakini sio kwa kasi ya kutosha. Usaidizi zaidi na ahadi zaidi zinahitajika.

- Nchi 171 kwa sasa zina angalau sera, mkakati au mpango mmoja wa kitaifa ya kukabiliana na hali hii. Kati ya hizi, asilimia 51 zina wa pili na asilimia 20 zina wa tatu.
- Nchi 16 kati ya 26 zisizo na chombo cha kitaifa cha kuweka mikakati zinatengeneza mojawapo, lakini nchi 10 hazionyeshi dalili yoyote ya kuunda chombo - 7 kati yake zimeanishwa kama za ngazi ya juu katika Fahirisi ya Nchi Dhaifu.
- Uwezekano wa ufanisi wa mipango ya kitaifa ya kukabiliana na hali (NAPs) kutoka nchi zinazoendelea umechanganyika na unaonyesha umuhimu unaoendelea wa kujitolea kwa dhati kwa mipango ya kukabiliana na hali katika nchi zinazoendelea.
- Hatua za kukabiliana na hali, licha ya changamoto kadhaa, zinaendelea kuongezeka. Hata hivyo, tathmini za miradi ya kukabiliana na hali inayofadhiliwa na taasisi za kutoa ufadhili chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) zinaonyesha kuwa takriban nusu yake sio ya kuridhisha au haiwezekani kuwa endelevu bila fedha za mradi kwa muda mrefu.
- Nchi zinaripoti hatua zilizopiga za utekelezaji wa NAPs zao, lakini nchi zote zilizotathmini utoshelevu na ufanisi wake ziligundua kuwa kiwango na kasi ya kukabiliana na hali haitoshi kwa kuzingatia hatari za tabianchi zinazoongezeka.

## Mambo wezeshi, mbinu mpya na vyombo vya kifedha ni muhimu kwa ufadhili wa kukabiliana na hali, kwa sekta ya umma na ya kibinafsi.

- Kwa sekta ya umma, viwezeshi hivi ni pamoja na uundaji wa mifuko na vyombo vya ufadhili, kuweka bajeti ya kushughulikia tabianchi na kuiwekea malengo maalum, kuyajumuisha katika mipango ya maendeleo ya kitaifa na mifumo ya matumizi ya muda fulani, na mikakati ya uwekezaji wa kukabiliana na hali.
- Mbinu mpya na asasi za kifedha pia zinajitokeza ambazo zinaweza kuimarisha ufadhili wa kukabiliana na hali. Hizi ni pamoja na fedha za kushughulikia hatari, asasi zinazohusishwa na bima, ruzuku zinazozingatia utendakazi, mikopo na dhamana ya ustahimilivu, madeni ya kushughulikia ukabilianaji wa hali na malipo ya huduma za mifumo ya ekolojia.
- Kwa sekta ya kibinafsi, uwekezaji unaweza kuhimizwa kupitia mifumo ya ufichuzi wa hatari za tabianchi, taksonomia za mabadiliko ya mikakati na kukabiliana na hali, na kwa kuimarisha mbinu na zana zinazohatarisha fedha za sekta binafsi kwa kutumia fedha za umma (fedha mchanganyiko). Hizi zinaweza kuungwa mkono na viimarishi na majukwaa ya kukabiliana na hali.
- Ongezeko linalohitajika katika mtiririko wa fedha za kukabiliana na hali linaweza kuungwa mkono na mageuzi yanayopendekezwa kwa taasisi za fedha za kimataifa na benki za maendeleo za kimataifa.

**Kukabiliana na changamoto za tabianchi kutahitaji kiasi kikubwa cha fedha za kukabiliana na hali na mbinu ya kimkakati zaidi ya uwekezaji. Pia ni sharti kuzingatia ni nani hatimaye hulipia kukabiliana na hali.**

- Ili kukabiliana na ukubwa wa changamoto za mabadiliko ya tabianchi, ufadhili wa kukabiliana na hali hii unahitaji kuacha kuzingatia hatua za muda mfupi, na zinazozingatia tu mradi na

kukabiliana na hali na kuanza kukabiliana na hali kwa kuzingatia uwezekano wa kutokea, mikakati na mabadiliko.

- Hii inahitaji hatua zaidi katika maeneo ambayo ni vigumu kufadhili. Kushughulikia ukabilianaji wa hali kama upunguzaji wa hali hiyo kutokea- yaani, kuzingatia maamuzi ya kiufundi, au kuzingatia maeneo rahisi zaidi kupata ufadhili tu - haitapelekea kiwango au aina za ukabilianaji wa hali unaohitajika.
- Swali la nani analipia ukabilianaji wa hali pia halijashughulikiwa vya kutosha. Katika mifumo mingi ya ufadhili, gharama kuu za kukabiliana na hali hubebwa na nchi zinazoendelea; hali hii inaweza kusaidia kuziba pengo la kifedha, lakini hairandani na kanuni ya majukumu ya kawaida lakini majukumu yaliotofautishwa na uwezo wake mtawalia, au na kanuni ya mchafuzi kulipia.

**Kujengea uwezo na uhamishaji wa teknolojia ni muhimu kwa uimarishaji wa ukabilianaji wa hali katika nchi zinazoendelea, lakini mabadiliko ya jinsi vinavyofanya kazi yanahitajika ili kuharakisha hatua za kukabiliana na hali nyanjani.**

- Kurejelea mahitaji ya uwezo na teknolojia kunapatikana kila mahali katika stakabadhi za UNFCCC, ikizingatia zaidi maji, chakula na kilimo. Hata hivyo, jitihada zinazoendelea za kukidhi mahitaji haya mara nyingi haziratibiwi, ni ghali na za muda mfupi.
- Sababu kadhaa hupunguza ufanisi wa uhamishaji wa teknolojia unaotolewa kwa sasa. Miongoni mwa yaliyoenea zaidi ni vikwazo vya kiuchumi na kifedha, kama vile gharama za juu za uwekezaji wa kwanza, ugumu wa kupata mikopo, na mifumo ya kisheria na ya udhibiti inayohitaji sera za ndani zinazosaidia zaidi ili kukuza na kuhamisha teknolojia na ujuzi unaotambuliwa kuwa muhimu na nchi zinazoendelea.
- Juhudi za kusaidia kujengea uwezo zinapaswa kutumia uwezo uliopo, kutoa msisitizo sawia kwa uwezo mgumu (teknolojia) na laini (hali wezeshi), na kutoa kipaumbele kwa usawa wa kijinsia na masuala ya ujumuishaji wa jamii.
- Ushahidi thabiti zaidi wa kuzingatia wakati wa kujengea uwezo na vipaumbele vya uhamishaji wa teknolojia vinahitajika, ikijumuisha kutoka kwa ufuatiliaji na tathmini. Hii ni pamoja na ushahidi kuhusu uwezo na mahitaji ya teknolojia, ambayo inashughulikia kazi ya vikundi tofauti vilivyoathiriwa, na gharama zao halisi.
- Mipango ya kujengea uwezo na uhamishaji wa teknolojia inapaswa kuunga mkono ukabilianaji wa hali katika sekta, viwango mbalimbali na vipaumbele vya maendeleo, na kuendesha mabadiliko chanya. Vipaumbele vya sasa mara nyingi ni vya kiufundi sana na vinalenga kushughulikia ahadi za kimataifa au majanga yaliopo, hali inayozuia juhudi za kuwa na mabadiliko ya kina.
- Mikakati ya kukabiliana na hali inapaswa kukuzwa kwa kuzingatia uelewa kamili wa mahitaji badala ya kutoka kwa mtazamo wa kusukuma teknolojia fulani, na kuifanya kuwa sehemu ya mikakati mipana ya maendeleo.